# MUHTASARI WA KIKAO CHA DHARULA CHA BODI YA ZABUNI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE KILICHOFANYIKA TAREHE 25/10/2021 KATIKA UKUMBI MDOGO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE

**A: WAJUMBE WALIOHUDHURIA** **MUHTASARI NO. 02/TB/2020/2021**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Omary Mungi | Kaimu Mwenyekiti | |
| 2. Bw: Victor Mwakapala | Katibu | |
| 3. Bw: Philipo Mwakibete | Mjumbe | |
| 4. Bw: Feliche Kigava | Mjumbe | |
| 5. Bibi: Emiliana C. Chamy | Mwanasheria | |

**B: WAJUMBE WASIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Bw. Gerald Kifyasi | Mwenyekiti - | kwa taarifa |
| 2. Bw. Auckland Hyera | Mjumbe - | Kwa taarifa |

**B: SEKRETARIETI**

| | |
|---|---|
| 1. Bw. Boniface Kijalo | Afisa Ugavi |

## DO.NA.11/BZ.2/2021/2022 – KUFUNGUA KIKAO

Kabla ya kikao kufunguliwa Katibu aliwasalimu wajumbe na kuwapongeza Wajumbe wapya walioteuliwa wa Bodi ya Zabuni ambao ni Bw. Omary Mungi na Bw. Feliche Kigava; baada ya utambulisho huo Katibu aliwaeleza Wajumbe kuwa kikao hicho ni cha dharula kwa ajili ya kujadili ajenda kuu tatu.

Aidha, Katibu aliwajulisha wajumbe wa kikao kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni Bw. Gerald Kifyasi na Mjumbe mmoja Bw. Auckland Hyera wapo kwenye shughuli Maalum za Mitihani. Kutokana na Mwenyekiti kutokuwepo alichaguliwa Bw. Omary Mungi kuwa Kaimu Mwenyekiti wa Kikao hicho kisha alimkaribisha Mwenyekiti ili aweze kufungua kikao. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kuhudhuria kikao hicho na kuwaomba kuwa makini katika kujadili ajenda zilizoandaliwa katika kikao hicho. Kisha alifungua kikao saa 02:16 asubuhi.

## DO.NA.12/BZ.2/2021/2022 – KUTHIBITISHA AJENDA ZA KIKAO

Katibu aliwasilisha kwenye kikao dondoo za ajenda kama ifuatavyo:-

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha agenda za kikao cha dharula cha Bodi ya Zabuni cha tarehe 25.10.2021.



CamScanner

3. Maombi ya idhini ya kuridhia ujenzi wa vyumba 55 vya madarasa na samani zake katika shule 18 za Sekondari kwa kutumia njia ya manunuzi ya "Force Account".
4. Maombi ya idhini ya kuridhia ujenzi wa vyumba 5 vya madarasa na jengo la Utawala kupitia TEA & EP4R katika shule ya Maalum ya Walemavu Katumba II pamoja na Ujenzi wa madarasa na vyoo katika Shule ya Msingi Lutete kwa kutumia njia ya manunuzi ya "Force Account" na ujenzi wa mfumo wa maji katika Shule za Msingi Bugoba na Ikukisya na Sekondari ya Kisondela kwa kutumia njia ya manunuzi ya "Force Account".
5. Maombi ya idhini ya kuridhia nukuu za bei kwa ajili ya ununuzi wa mfumo wa GOT HOMIS unaotarajiwa kufungwa katika Zahanati ya Kiwira.
6. Kufunga kikao.

**DO.NA.13.BZ.2/2021/2022 – MAOMBI YA IDHINI YA KURIDHIA UJENZI WA VYUMBA 55 VYA MADARASA NA SAMANI ZAKE KATIKA SHULE 18 ZA SEKONDARI KWA KUTUMIA NJIA YA MANUNUZI YA "FORCE ACCOUNT"**

Katibu aliwasilisha katika kikao maombi ya idhini ya ujenzi wa vyumba 55 vya Madarasa Katika shule za Sekondari kwa njia ya Manunuzi ya "Force Account".

Katibu alieleza kuwa katika dokezo la Idara ya Elimu Sekondari imeeleza kuwa Halmashauri imepokea fedha kiasi cha **Tsh. 1,100,000,000/=** kutoka TAMISEMI kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO -19 ikiwa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 55 vya Madarasa katika Shule za Sekondari ambazo zilikuwa na upungufu wa vyumba vya madarasa.

Katibu alieleza kuwa Halmashauri Wilaya ya Rungwe imepokea Fedha tajwa hapo juu kutoka IMF ikiwa ni kwa ajili ya kampeni ya mapambano dhidi ya Uviko 19 iliyozinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 10/10/2021 ambapo kila darasa limekadiriwa kukamilika kwa kiasi cha Tsh. 20,000,000.00 na kwamba kwa mujibu wa maagizo ya OR- TAMISEMI ujenzi unapaswa kukamilika kabla ya tarehe 15/12/2021 na kwamba Ofisi ya Mkuu wa Mkoa yenyewe iliagiza utekelezaji wa ujenzi wa madarasa hayo ukamilike kabla ya tarehe 30/11/2021.

Aidha, baada ya kuzinduliwa kwa kampeni hiyo Mamlaka ya Udhibiti Manunuzi ya Umma (PPRA) imesisitiza na kuagiza kutumia mzabuni mmoja katika ununuzi wa vifaa kupititia barua yake ya tarehe 12/10/2021 yenye kumbukumbu namba Ca. 192/211/01/74 kwa kuzingatia vifungu vya kanuni Na. 159,160 na 161 vya kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 kama zilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2016.

Hivyo basi, kwa maelezo yaliyotolewa hapo juu Katibu aliomba Bodi ya Zabuni ridhie ujenzi wa vyumba 55 vya madarasa katika Shule za Sekondari kutumia utaratibu wa manunuzi wa "Force Account".



CamScanner

Kikao kilipokea taarifa hiyo, kilijadili kwa kina ajenda hii na kuagiza kuzingatia maagizo yaliyotolewa na OR TAMISEMI na hatimaye kiliridhia ujenzi wa madarasa kutekelezwa kwa njia ya "Force Account".

**DO.NA.14/BZ.2/2021/2022 – MAOMBI YA IDHINI YA IDHINI YA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA, BWENI, VYOO NA MIUNDOMBINU YA MAJI KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI KWA NJIA MANUNUZI YA "FORCE ACCOUNT"**

Katibu aliwasilisha katika kikao maombi ya idhini ya kuridhia ujenzi wa vyumba 5 vya madarasa na jengo la Utawala kupitia Mamlaka ya Elimu (TEA) & EP4R katika shule ya Maalum ya Walemavu Katumba II pamoja na Ujenzi wa madarasa na vyoo katika Shule ya Msingi Lutete kwa kutumia njia ya manunuzi ya "Force Account" na ujenzi wa mfumo wa maji katika Shule za Msingi Bugoba na Ikukisya na Sekondari ya Kisondela kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya COVID -19 kwa kutumia njia ya manunuzi ya "Force Account".

Idara imeeleza kuwa Halmashauri imepokea jumla ya fedha kiasi cha Tsh **307,217,139.55/=** ambapo mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:-

(a) Ujenzi wa mifumo ya maji katika Shule za Msingi Bugoba na Ikukisya Tsh. 23,744,758.00 kupitia program ya UVIKO
(b) Ujenzi wa mfumo wa maji katika Shule ya Sekondari Kisondela Tshs. 11,872,379.85 kupitia program ya UVIKO
(c) Ujenzi wa Jengo la Utawala Tshs. 50,000,000.00 na Tshs. 40,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa kupitia EP4R katika Shule ya Msingi ya Mahitaji Maalum Katumba II
(d) Ujenzi wa madarasa matatu (3) Tsh. 60,000,000.00 kupitia Mamlaka ya Elimu (TEA) katika Shule ya Msingi ya Mahitaji Maalum Katumba II.
(e) Ujenzi wa Bweni la Wanafunzi Tsh. 80,000,000.00 katika Shule ya Msingi ya Mahitaji Maalum Katumba II kupitia COVID -19
(f) Ujenzi wa vyumba viwili(2) vya madarasa na matundu ya vyoo katika Shule ya Msingi Lutete kupitia Mamlaka ya Elimu (TEA).

Iivyo basi, kwa maelezo yaliyotolewa hapo juu Katibu aliomba Bodi ya Zabuni idhie utekelezaji wa miradi tajwa hapo juu kwa njia ya manunuzi ya "Force ccount".

ikao kilipokea taarifa hiyo; kilijadili kwa kina kiliagiza kuzingatia taratibu za anunuzi katika utekelezaji na kisha kiliridhia njia ya manunuzi itakayotumika ıtika utekelezaji wa miradi tajwa hapo juu.

**).NA.15/BZ.2/2021/2022 – MAOMBI YA IDHINI YA KURIDHIA UNUNUZI WA FAA KWA AJILI YA MFUMO WA GOT-HOMIS KATIKA ZAHANATI YA KIWIRA**

Katibu aliwasilisha katika kikao, maombi ya idhini ya ununuzi na ufungaji wa vifaa vya mfumo wa GOT- Homis kwa ajili ya Zahanati ya Kiwira. Alieleza kuwa Kitengo cha Manunuzi kimepokea maombi haya kutoka Idara ya Afya ikieleza kuwa Zahanati ya Kiwira inategemea kufunga mfumo kwa ajili ya kuthibiti uingiaji na utoaji wa dawa katika zahanati hiyo.

~~Katika~~ Katibu alieleza ~~katika~~ katika kikao kwamba Idara Afya kuwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 imetenga fedha kwa ajili ya kufunga mfumo huo. Fedha hizo zitalipwa kupitia mfuko wa Health Sector Basket Fund- (HSBF) kufuatia maombi haya Zahanati ya Kiwira ilifanya ushindanishi mdogo wa nukuu za bei ya vifaa vya GOT – HOMIS na kwamba baada ya ufunguzi wa nukuu hizo na kukokotolewa majibu yalikuwa kama ifuatavyo:

| Na | Jina la Mzabuni | Kiasi | Msimamo |
|---|---|---|---|
| 1 | Jubela General Company Ltd | 9,949,500.00 | 2 |
| 2 | Biazo Tsalach Technologies | 9,203,000.00 | 1 |
| 3 | One Man Group | 14,229,500.00 | 3 |

Hivyo basi, kwa maelezo yaliyotolewa hapo juu Katibu aliomba Bodi ya Zabuni iridhie maombi ya Idara ya Afya vya vifaa vya GOT – HOMIS kununuliwa kupitia kwa mzabuni M/s Biazo Tsalach Technologies kwa gharama ya Tshs. 9,203,000.00

Kikao kilipitia kwa kina maamuzi yaliyofanyika na kuridhia ununuzi wa ~~vya~~ vifaa vya GOT – HOMIS kununuliwa kupitia kwa mzabuni M/s Biazo Tsalach Technologies kwa gharama ya Tshs. 9,203,000.00 na kuhakikisha Kitengo cha Manunuzi kifanye ukaguzi wa mapokezi ya vifaa hivyo.

**DO.NA.16/BZ.2/2021/2022 - KUFUNGA KIKAO**

Kabla ya kikao kufungwa, Katibu aliwashukuru wajumbe kwa kuhudhuria kikao hicho muhimu, kisha alimkaribisha Mwenyekiti kwa ajili ya kufunga kikao. Mwenyekiti aliwashukuru sana wajumbe kwa kuitikia kikao hicho na alisisitiza kutekeleza maagizo yote yahusuyo miradi tajwa hapo juu kwa kuzingatia taratibu za Manunuzi ya Umma; kisha Mwenyekiti alifunga kikao saa 03:25 asubuhi.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA:**

| | |
|---|---|
| ................................ | ................................ |
| **OMARY MUNGI** | **BW: VICTOR A. MWAKAPALA** |
| **KAIMU MWENYEKITI** | **KATIBU** |

**TAREHE:** ......26/11/2021.......